



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE



Kumb.Na.KTV/MLDC/S.10/12

07.08.2024

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele amepokea kibali cha Ajira mpya kwa ikama ya mwaka 2023/2024 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora chenye **Kumb.Na.FA.97/288/01/09** cha tarehe **25/06/2024**. Hivyo, anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenyе sifa za kujaza nafasi ifuatayo:-

1.0. MPISHI DARAJA LA II (NAFASI 03)

1.1.1 KAZI NA MAJUKUMU

- i. Kufanya usafi wa jiko;
- ii. Kupika vyakula vya aina mbalimbali;
- iii. Kuhakikisha vyombo vya kupikia vinakuwa safi
- iv. Kutayarisha orodha ya vyakula vya mlo kamili (balanced diet);
- v. Kupika vyakula vya kitaalam;
- vi. Kuhakikisha chakula kinaandaliwa kwa muda muafaka;
- vii. Kuahakikisha usalama wa jiko na chakula; na
- viii. Kutekeleza majukumu mengine utakayopangiwa na msimamizi wako

1.1.2 SIFA ZA MWOMBAJI.

Awe amehitimu kidato cha nne (IV) au kidato cha sita (VI) na kupata cheti cha Mthani wa Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI). Awe na Astashahada/cheti (Technician Certificate) ya fani ya Mapishi (Food Production/ Culinary Arts) kutoka Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

1.1.3 NGAZI YA MSHAHARA

Kwa kuzingatia Ngazi za mishahara ya Serikali **TGS C**

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- i. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania na wenyе umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45 isipokuwa wale waliokokazini Serikalini;
- ii. Waombaji wenyе ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuhainisha kwenye Mfumo wa kuombea ajira ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;
- iii. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detail Curriculum Vitae) yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na Anuani ya Barua Pepe (E-mail address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.
- iv. Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma na wamejipatia Sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitishe barua zao za maombi yanafasi ya kazi kwa waajiri wao na waajiri wajiridhishe ipasavyo;
- v. Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu naTaaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne au Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika. **Certificates, - Cheti cha mtihani wa Kidato cha IV na VI,-Computer Certificate;**
- vi. “Testmonial”, “Provisional Results”, “Statement of results”, hati ya matokeo ya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita (**FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS**) **HAVITAKUBALIWA.**
- vii. Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na vimethibitishwa na Mamlaka husika (**TCU, NECTA na NACTE**).
- viii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi;

- ix. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka **Na. CAC.45/257/01/D/140** watarehe **30 Novemba,2010**.
- x. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- xi. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **14 Agosti, 2024**.
- xii. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazii liyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, anuani ya barua hiyo ielekezwekwa:-

Mkurugenzi Mtendaji,

Halmashauri ya Wilaya ya Mlele

**S.L.P 686,
Mpanda – Katavi.**

- xiii. Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo; <https://portal.ajira.go.tz/> (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu ilioandikwa ('Recruitment Portal')).
- xiv. **Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.**

Tangazo hili limetolewana :

Sigilinda M. Mdemu

**MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE**

